# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Aidha, nachukua nafasi hii adhimu kukushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Spika** kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza baraza hili tukufu kwa weledi na uadilifu wa hali ya juu. Tunaamini kuwa utaendelea kuliongoza baraza hili kwa umakini kwa lengo la kuendeleza demokrasia katika taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna anavyoiongoza nchi yetu na hatua mbali mbali anazozichukua za kutuletea maendeleo kwa kuanzisha miradi mbali mbali ambayo kukamilika kwake kutawanufaisha wananchi wetu. Pia niwapongeza Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa mchango mkubwa wa muongozo na mawazo ambayo yanasaidia katika kuiongoza nchi yetu vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhan na hatimae kusherehekea sikukuu ya Eid El fitr kwa salama na amani.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wake wote kwa jitihada kubwa wanazozichukuwa katika kuiletea nchi yetu maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa kutekeleza vyema majukumu yao ipasavyo kwa kipindi chote cha Kamati, jambo linalonipa mimi wepesi wa kuiongoza

Kamati hii inayosimamia masuala muhimu sana katika nchi yetu. Wajumbe hawa wamekuwa makini muda wote na waliitumia taaluma na uwezo wao katika kutoa michango wakati wa uwasilishwaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, kwa lengo la kuhakikisha kuwa, sekta ya biashara na viwanda zinaimarika na kupiga hatua kubwa katika kuiletea nchi yetu maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yussuf Hassan Iddi | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Aza Januari Joseph | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Said Saleh Salim | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii inafanya kazi zake kwa msaada mkubwa wa makatibu wetu wawili ambao ni :-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 2. | Ndg. Mwaka Mwinyi Wazir | Katibu |

**Mheshimiwa Spika**, Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kila mwaka wa fedha, kama Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ilivyoelekeza. Katika kulitekeleza jukumu hili, Kamati ilikutana na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanza kuelezea Makadirio hayo kwa Programu za Wizara hii, kwa ruhusa yako naomba nichukuwe nafasi hii kuelezea maoni ya Kamati kuhusiana na Mapato ya Wizara kwa mwaka wa fedha uliopita 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni **2.84** kupitia vyanzo

vyake mbali mbali, Wizara imejipangia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 1.7 hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ambapo hadi kufikia mwezi wa Febuari 2022, Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni **1.75** sawa na **101** % ya makadirio ya makusanyo hayo, fedha ambayo kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati ilipelekwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haipingani na sheria na kanuni zetu tulizojipangia kuhusiana na suala la kupeleka fedha katika mfuko mkuu wa Serikali, lakini inahisi kuwa suala hilo utaratibu wake usipofanyiwa marekebisho kutokana na mahitaji tuliyonayo kwa sasa katika taasisi zetu, tutaendelea kuwa na changamoto nyingi kwa taasisi zote zinazofanya makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali halisi tuliyoikuta katika baadhi ya taasisi tulizozifanyia ziara, tunachukua nafasi hii kuishauri Serikali kufanya marekebisho katika baadhi ya sheria endapo sheria inaelekeza hivyo, ili mapato yanayokusanywa na taasisi zetu yabakie katika taaisi hizo kwa asilimia kadhaa ambayo yatasaidia katika utatuzi wa changamoto mbali mbali zilizopo kwa sasa.

**Mheshmiwa Spika**, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilijipanga mipango mkakati ambayo haikuweza kutekelezeka kutokana na changamoto ya ukosefu wa fedha. Baadhi ya mipango iliyoshindwa kutekelezeka ni pamoja na mpango wa uendelezaji wa miradi ya kimkakati, kutokana na ukosefu wa fedha na hiyo fedha iliyokusanywa iliingia yote katika mfuko Mkuu wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa matumizi, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi **bilioni 30.54** kwa ajili ya kutekeleza Programu zake Kuu tatu, kati ya fedha hizo shilingi **bilioni 5.3** tu ambazo ni sawa na **20%** ndizo zilizoingizwa hadi kufikia mwezi Machi 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imesikitishwa sana kuona kiwango kidogo cha fedha zilizoingizwa kwa matumizi ya Wizara hii kwa mwaka huo wa fedha. Uingiaji huo wa fedha haulingani kabisa na shughuli kubwa zilizopangwa kufanyika. Kutokana na hali hii, Kamati inaonesha wasiwasi wake kwa makadirio madogo ya fedha iliyotengwa kutumika kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kwamba inaweza kukwamisha kabisa utekelezaji wa shughuli nyingi zinazotarajiwa kutekelezwa na Wizara hasa tukichukulia uzoefu wa uingizwaji mdogo wa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Raisi, fedha na Mipango kuwaingizia kiwango cha fedha kilichosalia kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kabla ya kuingiza bajeti ya mwaka huu wa fedha, lengo hasa ni kuiwezesha Wizara hii kufikia malengo iliyojipangia.

**Mheshmiwa Spika,** Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepangiwa kutekeleza Peogramu Kuu nne (4) kama ifuatavyo:-

i) Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara;

ii) Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali;

iii) Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara;

iv) Programu kuu ya Viwango na Tathmini ya Ubora.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA

**Mheshimiwa Spika**, programu hii inajumuisha programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba, ambayo inajukumu la kusimamia shughuli zote za Wizara ya Biashara kisiwani Pemba. Kamati imesikitishwa sana na upunguaji wa fedha za makadirio katika fungu hili ukilinganisha na fedha za makadirio ya bajeti iliyopita. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii imekadiriwa kutumia shilingi **2,977,527,000** wakati bajeti iliyopita fungu hili lilipangiwa kutumia shilingi **3,037,903,000.** Kamati inaamini kuwa kupungua kwa fedha hizi kutakwamisha utekelezaji wa malengo mazuri ya Wizara ambayo yanalenga kuwasaidia wananchi moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiingizia Ofisi hii fedha hizo kwa wakati ili waweze kufanikisha majukumu ya taasisi zilizo chini ya Ofisi hii.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

**Mheshimiwa Spika**, programu hii utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (SMIDA), ikijumuisha programu ndogo mbili ambazo ni programu ndogo ya ukuzaji wa viwanda pamoja na programu ndogo ya maendeleo ya wajasiriamali.

**Mheshimiwa Spika**, sote ni mashahidi kwamba nchi yetu ina malengo mazuri katika kufikia uchumi wa viwanda utakaotuwezesha kujitegemea kwa asilimia kubwa katika mipango, makusanyo na matumizi ya fedha zetu wenyewe. Baada ya kupitia bajeti hii, Kamati imebaini kwamba Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ina mipango mizuri itakayosaidia kufikia hatua hiyo ikiwa ni pamoja na kuyaendeleza maeneo ya viwanda ya Dunga na Pangatupu kwa kuyapima, kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi, kulipa fidia kwa wananchi, kufikisha miundombinu ya umeme, maji pamoja na kutengeneza barabara za ndani, pamoja na maeneo ya maonensho ya kibiashara ya

kimataifa Nyamanzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini changamoto ya kupungua kidogo kwa bajeti inayokadiriwa kutumika kwa miradi hii ya maendeleo. Jumla ya shilingi **11,600,000,000** iliyopangwa kutumiwa na Wizara hii kwa mwaka wa fedha **2022/2023** kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha sekta ya viwanda nchini. Kamati inaamini kuwa endapo feha hizi zitapatikana kwa wakati upungufu mdogo uliojitokeza katika makadirio haya hautaathirisana utekelezaji wa miardi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaizidi kuishauri Serikali kuingiza kwa wakati fedha hizo ili Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda itekeleze majukumu yake kwa ufanisi pamoja na mbinu mbali mbali Wizara itakazozibuni za kuingia ubia na wawekezaji binafsi pamoja na washirika wa maendeleo kwa lengo la kupata fedha zitakazoweza kuiimarisha na kuiendeleza sekta hii ya viwanda .

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaipongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa juhudi ilizozichukuwa na kufanikiwa kuanza maandalizi ya ujenzi wa kiwanda cha mwani.Pia tunapongeza kuanza kazi kwa kampuni ya mwani baada ya kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mtendaji, tunaamini kuwa huu ni mwanzo mzuri ambao utawasaidia wananchi wetu kujiimarisha kiuchumi hasa wakulima wa mwani ambao wengi wao ni wakipato cha chini.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa sekta hii, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa zao la mwani kwa lengo la kuongeza kasi ya uzalishaji wake, ili kiwanda hiki kitakapomalizika kiweze kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa Wizara ya Biashara ndio inayobeba uchumi wa nchi yetu ukiachana na Utalii ambao unaonekana kukumbwa na changamoto kadhaa kama vile mlipuko wa maradhi ya Covid 19 ambayo yaliutikisha uchumi wa dunia ikiwemo Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali izidishe juhudi zaidi katika kuiendeleza sekta ya **viwanda na biashara**. Kamati inaamini kuwa endapo Serikali itaandaa mazingira mazuri ya kuzikuza kikamilifu sekta hizi, zitaweza kutunyanyua na kupunguza makali ya muelekeo wa anguko la uchumi kwa taifa letu.

## PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

**Mheshimiwa Spika**, programu hii inalenga kuimarisha nafasi ya Zanzibar katika usafirishaji wa bidhaa na masoko ya Kikanda na Kimataifa. Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa malengo yake imara iliyojipangia kwa mwaka ujao wa fedha **2022/2023** kwa kuanzisha na kuendeleza sekta ya **TEHAMA** ya

viwanda nchini ambayo inalenga kusaidia upatikanaji wa taarifa muhimu katika kufikia malengo ya uchumi wa viwanda. Aidha mfumo huu utasidia katika kutanua wigo wa upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zetu ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuyafanikisha malengo haya, Kamati inaishauri Wizara kujipanga katika kuhakikisha kuwa inapata wataalamu wa kutosha wa kuuendesha mfumo huu ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa. Kamati inaamini kuwa mfumo huu ni muhimu sana katika kuisaidia Wizara kwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknologia iliyopo duniani hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Malengo hayo mazuri ya Wizara iliyojipangia kwa mwaka wa fedha **2022/2023** yanaweza kushindwa kutekelezeka kutokana na uhaba wa fedha iliyokadiriwa kwa programu hii. Jumla ya shilingi **9,685,951,000** zimekadiriwa kutumika kwa programu hii, fedha ambayo Kamati inaiona ni ndogo mno ukilinganisha na fedha iliyokadiriwa kwa mwaka wa fedha uliopita ambayo ilifikia shilingi **bilioni 13,785,424,000.**

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uhaba huo wa fedha, Kamati inaishauri Serikali kuviangalia upya vipaumbele vya nchi ili tuweze kufika tunapopataka. Kamati inayasema hayo kutokana na fedha ndogo iliyotengwa ambayo inalenga kukuza na kuendeleza biashara. Tunaamini kuwa fedha hiyo ni ndogo sana kutokana na kukuwa kwa teknolojia duniani pamoja na mahitaji na ushindani mkubwa uliopo hivi sasa katika sekta ya biashara.

**Mheshimiwa Spika**, programu ndogo ya Uwezeshaji wa Biashara kupitia Huduma ya Uimarishaji wa Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji inakazi kubwa ya kufanya kwa sasa, kutokana na changamoto kubwa ya kupanda kiholela kwa bei za bidhaa muhimu nchini, hali inayowaathiri wananchi walio wengi ambao ni wenye kipato cha chini.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Wizara kuchukuwa hatua za makusudi katika kuwafuatilia wafanyabiashara juu ya utekelezaji wa bei elekezi zilizotolewa na Serikali kwa lengo la kumlinda zaidi mtumiaji ili aweze kupata unafuu wa maisha.

## PROGRAMU KUU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Taasisi ya Viwango Zanzibar kwa kutekeleza vyema majukumu yake kwa mwaka wa fedha uliopita. Hata hivyo Kamati inaishauri Taasisi hii kuongeza nguvu katika kuwafuatilia wafanyabiashara ili kuhakikisha kwamba, bidhaa wanazoziingiza sokoni zina viwango na ubora kwa afya za watumiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Suala la uimarishaji wa viwango vyetu vya ndani ni jambo la msingi kufanyiwa kazi na Wizara hii, kwani kadri nchi yetu inapoviidhinisha viwango ndipo

itakapopata fursa ya kutanua wigo wa usalama wetu kupitia bidhaa na vifaa tunavyovitumia. Kamati inaisisitiza Wizara kuhakikisha viwango vinavyoandaliwa viko sahihi na vinakubalika na Taasisi za Viwango za kimataifa hasa tukizingatia kwamba, ulimwengu tayari umekuwa sawa na kijiji kutokana na kukuwa kwa sayansi na teknolojia.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

**Mheshimiwa Spika**, moja kati ya majukumu ya msingi ya Shirika hili ni kuuza na kununua karafuu na mazao mengine ya viungo nchini. Kamati inachukuwa nafasi hii kulipongeza Shirika hili kwa kununua jumla ya **tani 8,703** za karafuu kwa msimu uliomalizika kwa shilingi **bilioni 113.6**, ambazo ni sawa na **202%** ya Makadirio kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Serikali kupitia Shirika hili kuimarisha ukulima wa zao la karafuu kwa kuwapatia wakulima wa karafuu miche bora na kwa wakati. Kwa mnasaba huu, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kushirikiana kikamilifu na Wizara ya Kilimo, kwa lengo la kuotesha miche hiyo ili kuondosha usumbufu wa upatikanaji wa miche pale msimu wa kilimo unapowadia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza hatua iliyochukuliwa na Shirika ya kubunifu Mradi wa Ujenzi wa Maghala ya ZSTC yaliyopo Madungu Chakechake Pemba. Mradi huu ujenzi wake ulianza mwaka wa fedha 2018/2019 unaohusisha Maghala matatu, jengo la uwekezaji, eneo la maduka, jengo la Benki, kituo cha manunuzi ya karafuu na maeneo ya maegesho ya magari. Aidha, mradi ulikisiwa kugharimu kiasi cha shilingi **7,246,300,328.95** za kitanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata nafasi ya kutembelea katika eneo la mradi huu na kubaini changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na ile ya kukosekana kwa fedha, hali iliyopelekea kusimama kwa ujenzi wa mradi huu takribani kwa kipindi cha mwaka mzima. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa mbele ya Kamati, Ujenzi wa mradi huu ulisimama tokea mwezi wa Novemba 2020 hadi mwezi wa Disemba 2021, ambapo Shirika la ZSTC lilishindwa kumlipa Mkandarasi fedha kwa wakati kama mkataba unavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,**Kutokana na hali halisi ya upatikanaji wa fedha, Kamati inaendelea kutoa rai kwa Wizara na taasisi zake kuendelea kuwa wabunifu katika kutafuta vyanzo vyengine vya fedha ikiwa ni pamoja na kuunga mikataba na washirika mbalimbali wa maendeleo duniani kwa lengo la kuhakikisha kuwa, malengo yaliyopangwa na Wizara yanatekelezeka kwa wakati. Aidha Serikali nayo kwa upande wake tunaishauri iongezee fungu la bajeti ya kutosha kwa Wizara hii kupitia taasisi na mashirika yake ili mwisho wa siku Wizara iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi mkubwa.

HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusiana na bajeti ya Wizara hii ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Niwashukuru pia wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa. Sasa niwaombe wajumbe wako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii, kwa lengo la kumuwezesha Mheshimiwa Waziri, kuyatekeleza kwa ufanisi yale yote waliyojipangia kwa mwaka wa fedha unaokuja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii naunga mkono hoja hii kwa 100%.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**Ahsante sana,**

……………………………………

**Yussuf Hassan Idd,**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**Zanzibar.**